# Tusi jipya

ABYAS MZIGUA

## NENO LA MWANDISHI

RIWAYA hii imeandikwa kwa misingi ya tafsida. Muundo wake ukiwa umebeba dhamira ya kiutu uzima. Baadhi ya maneno yanaweza kuwa yenye kukera kwa kundi fulani la watu. Ukiwa wewe ni mmojawapo, basi unapokutana na hali hiyo unashauriwa ukifunge kitabu hiki na kuendelea na shughuli nyingine.

Pia, mtambao wa lugha uliomo humu ni mtamu sana. Mwandishi kabeba zana zote za tamathali za semi kuifanya kazi ibebe ladha ya asali, hivyo kuna uwezekano ukakimaliza kitabu na kutamani uwe nd'o unakianza.

Ahsanteni.

Mimi ni ABYAS MZIGUA
WhatsApp: 0688589070
Email: abyasmzigua@gmail.com
Dar Es Salaam, Tanzania.

# 1

Nyingi zikaenda, za kubaki zikasalia. Siku zikasonga, walio hai wakapumua. Anga zikafunga, mvua kushangilia. Jua lilipopunga, radi zikakimbia. Bado mitaa ya Manzese ilibaki kama ilivyo, hakuna ambacho kilibadilika kwa hali yoyote iliyojaribu kutishia. Watu walizikumbatia tamaduni zao na hawakuwa tayari kuziachia. Akaja mwanalaana kutoka huko alikokuwa... Suzi binti Chitete!
Hili jina litaje bila kufikiria. Alikuwa mgeni aliyefanya wenyeji wote kuchukia. Labda utasema namuonea. Tega umakini nianze kukusimulia...

Mwanzo alikuwa ni msichana tu aliyekuja kama mpangaji. Akachukua chumba kimoja. Lakini hakuwa na hata sufuria. Aliingia hivyo alivyo. Hakuna ambaye alimzingatia, ilimradi mwenye nyumba alipewa stahiki yake, hata jina lake la pili hakuliulizia. Kodi ya miezi sita kwapani, jina kitu gani? Hata kunguru na mende nao wana majina bwana!

Suzi akapata hifadhi. Taratibu akaanza kujikusanya. Alisomba kitanda, akasogeza vyombo vichache, mwishowe makabati mpaka yaliyokosa vitu vya kuhifadhia. Hakuna ambaye alimjua msichana huyu kiundani. Wapangaji wenzake, kitu pekee walichokuwa wakipokea ni salamu tu ya asubuhi. Wangedai pesa ya umeme wangepatiwa, wangetaka mchango wa maji wangekabidhiwa. Labda zamu ya usafi, wangekuta kumeshanadhifiwa. Suzi alikuwa ni mtu wa mambo yake. Ya watu aliwaachia wenyewe. Angetoka asubuhi akarudi nyakati ambazo tayari jua limeshayabusu mawingu. Baada ya hapo, asingeonekana tena mpaka asubuhi nyingine ya kufuatia.

Debe tupu haliachi kuvuma! Litapiga kelele lisikike kila kona. Suzi alikuwa ni debe lililosheheni, hakuvuma, msichana mkimya na mtaratibu. Wengine wakafikia kudhani ni msichana wa serikali. Yumkini ni mpelelezi. Hawa wakamhanya. Walimuogopa.

Hakujali yasemwayo. Akabaki na ukweli uliokuwa ukiishi katika moyo wake, ukweli asiotamani yeyote kuusikia. Aliufanya siri.

Enhee, siri!

Lakini siri ipi inayoishi ndani vyumba nane vya nyoyo mbili? Ama tatu..... Nne...?
Haipo!
Siri inayobebwa na watu wawili na kuendelea, huwa na tabia ya kipekee. Kufa na kufufuka. Kifo cha siri hushamiri utakatifu wa ahadi na viapo vya kuvutia. Na siku ya kufufuka husaka wa kumvamia bila kuchagua. Na hairidhi mmoja, itatafuta umati wa kuipokea.
Akheri ya 'Masiha' atafufuka kwa dalili, siri haina hiyo sifa, si saa tatu si saa mbili. Itakuja tu. Bila ya kutegemewa.
Kama ambavyo Suzi alivyokuwa ametulia zake siku hiyo. Mchana. Ukaja ugeni. Ugeni wenye matarumbeta na vipaza sauti. Wanawake waliovaa sare walimwaga radhi bila kujali atakayeziokota. Walicheza kwa kujiachia. Maungo yote wazi. Msafara wao ukapata watazamaji. Waume kwa wakike. Hawa wakike nao walijiunga kuviburudisha viuno vyao. Waume waliunga nao pia, ila hawa waliyaburudisha macho yao. Burudani juu ya burudani, burudani iliyosomba kijiji!
Kituo kikawa anapoishi Suzi.

Suzi akatolewa ndani. Wakazi wa mtaa hawaamini walionalo. Suzi binti mkimya kamkosea nani huyo mwenye roho mbaya? Binti mstaarabu, kamkwaza nani huyo aliyenyimwa nyama ya kusamehe?
Walijiuliza huku wakibaki mashuhuda. Jiingize ujifanye kutetea upepo ukugeukie wewe!
Nani sasa yu radhi kuumbuliwa?
Suzi alikosa mtetezi.
Ubavu mweusi wa Suzi uliokuwa haufahamiki pale mtaani, ukapinduliwa. Uliwekwa wazi. Kumbe kazi yake ni chafu isiyotamkika. Anauuza mwili wake kwa furusi za kuhesabika. Nd'o kibarua chake, kimwekacho mjini. Na wale waliomfungia msafara, walikuwa ni wanawake walioungana kwenda kumchamba, kwenda kumshushua, kumsuta kama inavyoitwa, kwa tabia yake ya wizi wa wanaume wa watu. Huyu akatoka mbele akadai kapokonywa mume, yule akapiga kelele kulalamika Suzi kambebea bwana. Ili mradi ni malalamiko dhidi ya Suzi. Suzi mbeba vya watu. Majirani vinywa wazi, wapangaji wenzie miguno ya kukataa kuamini ikatamalaki. Suzi wanayemsikia na Suzi waliyekuwa wakiishi naye ni viumbe wawili ambao hawawezi kuketi meza moja wakaongea.

Hakika lilikuwa gumzo. Kile kigoma kiliondoka kikaacha fadhaa na hadaa mtaani.

Suzi hakutazamika. Sasa sifa ya fisi aliyejiveka ngozi ya kondoo ikamwandama. Akanyooshewa vidole kila alipokatiza. Wakazi wa mtaa ule uliopo Manzese ikawa nd'o mada ya kunogesha umbea walipokuwa kwenye vikao vya mbacha zao. Mdada mpole kumbe ana siri kubwa. Hakika usimtazame mtu kwa nje, moyo wa mtu msitu. Ndiyo walivyokuwa wakisema wakazi hawa. Hasa wanawake. Wakasahau kuwa na wale waliokuja kupiga kelele ni wanawake kama wao.

Na labda, aidha kwa kufanya kusudi, ama kwa kupitiwa, wakashindwa kutambua kuwa wenzao walishanyolewa, basi wangepaswa na za kwao wazitijie maji...

Labda walisahau. Pengine.

Ila yeye Suzi hakuwa na muda wa kufanya ujinga huo. Ujinga wa kusahau kuwa tayari ubaya wake ulishatangazwa, hivyo kuuficha ingekuwa ni kazi bure. Hakutaka tena kubeba matendo mema ilihali uovu wake unajulikana na kila mmoja.

Teyari alishavuliwa nguo na kila mlimwengu kuiona tupuye, achutamie nini sasa?

Eti?

Achutame kwa ajili gani? Kipi akifiche ambacho hakijaonekana?

Balaa likaanza kwa baba mwenye nyumba, akampa ladha ya tunda la mti wa kati. Akahamia kwa wapangaji, mlango kwa mlango, wote wakailamba asali kwa ukubwa wa vidole vyao. Na waliotamani kurudia kuchovya hawakukatazwa.

Suzi Chitete katika ubora wake!

Mwendo kama wa ngamia aliyeishiwa mafuta katika nundu, utaratibu wa kuongea na midomo yake myekundu, huko nyuma akaumuka utasema ni manundu. Sisemi kuhusu kitandani sasa, alivyo mtundu, anatoa mpaka.....

Anatoa mpaka gundu!

Ndiyo, unaweza kujihisi una bahati kuliko wanaume wote katika sayari hii. Na hiyo nd'o silaha yake kuu ya maangamazi. Humpata anayemtaka tena kwa haraka.

Mitego yake ni ya uhakika.

Mpaka muda huo hakuna aliyekuwa akimjua binti huyu atokeapo, wala historia yake. Na ule moto wa vifuu uliokuwa ukipitia wanaume katika nyumba ya wapangaji, ulimaliza kazi yake na kuacha majivu.

Shutuma zilishaanza kusikika. Wanawake walilalamika. Suzi kaanza wizi.

Katikati ya shutuma hizi, zikaibuka nyingine nazo kutoka mtaani, kwa majirani... Lalamiko ni lilelile, Suzi mlowezi wa wanaume na fisadi wa mapenzi ya wenzie. Yakamfikia mwenye nyumba. Naye kuepusha zahma, akamwandikia barua ya uhamisho. Baada ya wiki mbili, Suzi alisomba kila kilicho chake na kuondoka.

Nyuma akaacha kumbukumbu ya jina lake. Ikitumika kwa mfano pale wamama walivyohitaji kuonya mabinti kwa tabia zao za usiri kumbe kuna mambo wayafanyayo. Na wale ambao waliiba wanaume wasiowahusu wakaitwa kwa jina hilo hilo. Suzi Chitete! Hakuna ambaye aliitwa Suzi Chitete akafurahia. Na ikibidi ugomvi kabisa kumwagika. Lilikuwa jina baya. Lisilopendeza. Tusi.

Halafu, sifa ya tusi, hasa kwa yule anayetamkiwa na asilifahamu, linaweza kuwa neno la kumpendeza na akalifurahia.

Huko alikoelea Suzi, alikwenda kuwa tusi jipya. Wenyeji hawakulifahamu. Wakalipokea huku wakitabasamu.

Tabasamu la idadi kamili ya meno katika vinywa vyao...

# 2

Hii ni hadithi. Hadithi inayoanzia Mwanza, katikati ya viunga vya jiji hilo. Ambapo binadamu wawili walikutana kwenye nyakati za udogo wao. Kijana Elia akiwa ni mtoto wa mwenye nyumba, huku Tausi ni mtoto wa mpangaji. Wote walikuwa ni wanafunzi wa shule ya msingi Nyamagana, shule iliyopo hukohuko, Mwanza.

Tausi darasa la tano; Elia akikaribia kuimaliza elimu yake ya msingi, akisubiri kuketi katika mtihani wake wa mwisho, mtihani wa Taifa wa darasa la saba. Ukaribu wao ukanatishwa kwa namna walivyokuwa wakishirikiana katika masomo licha ya utofauti wa madaraja uliokuwepo. Heshima kubwa kabisa ikaota mbawa baina yao. Majina 'kaka' na 'dada' yakavizoea vinywa vyao.

Kikombe hiki cha udugu usio wa damu kikaja kuvunjwa na maamuzi ya muda. Muda uliamua. Elia akachaguliwa kuja kusoma jijini Dar Es Salaam,

kwenye shule ya Sekondari Azania. Shule ya mjini, shule ya wavulana ya kutwa. Tausi akasalia hukohuko Mwanza.

Kupotezana huku kukazidi kukita mizizi, pale Elia alipotakiwa kuendelea na masomo yake ya kidato cha sita kwenye shule hiyohiyo.

Na kwa vile jiji lilikuwa limemnogea, hata likizo ilipotokea haikutosha kumkumbusha kuhusu mahala alipozaliwa na kukua.

Ilidumu hivyo mpaka alipofika chuo. Kipindi ambacho masomo yalimsogezea upenyo, au labda alishalikinai jiji la Dar Es Salaam, taratibu akawa na visafari vya kushtukiza kuelekea Mwanza. Visafari vifupi, vya siku zisizozidi tano.

Mmmh! Kwa upi huo, hapana! Huyu bado hakuwa amelichoka jiji. Mnisamehe kwa kuwadanganya.

Lakini, katikati ya ufinyu huo, katikati ya muda ambao hakuutegemea, Elia anakutana upya na sura iliyokaribia kumpotea, Elia akakwaana na Tausi. Hawakusahauliana. Wakabadilishana nambari za simu. Wote wakiamini yalikuwa ni makutano ya dada na kaka wa utotoni.

Wakasahau kuwa tayari walishapevuka. Mazoea yalipomea katika vichwa vyao, majina rasmi yakabadilika. Pale Tausi alipomuita mwenzake 'mpenzi' kwa kudeka, Elia angetabasamu na kusema 'Naam malaika'. Hatimaye, ule urefu wa safari za Elia ukaongezeka. Na zisingekuwa za ghafla tena... Angefika Mwanza kwa kupanga, akakutana na mapokezi ya kumtoa mawazo ya masomo yake kichwani... Mapokezi yaliyokamilika.

Kopa lao lililokuwa limejaa wekundu usiomithilika, halikutaka kukubali lisalie tu kwenye kelele za mitikisiko ya vitanda, likahamia kwenye uzito wa mifuko yao. Tausi akageuka mshauri mzuri wa kiuchumi kwa Elia. Akamuonesha fursa ya mafanikio. Alimshawishi wafanye biashara ya usafirishaji samaki kutoka Mwanza kwenda jijini Dar Es Salaam.

Ikawa hivyo.

Mwanza yuko Tausi, Dar Es Salaam yuko Elia. Hawa wakawa wasimamizi wa kujitegemea. Biashara ikasimama mbele ya changamoto lukuki. Elia sasa akawa kijana mwenye pesa za kutosha na kujitegemea.

Akamaliza chuo... Wakaoana... Lakini biashara haikubadili mwenendo wake... Kampuni ikakua. Ikaingia mikataba ya kusambaza samaki katika maduka makubwa na 'supamaketi'. Namna za usafirishaji zikawa bora na kufikia kutumia ndege. Hawakuwa samaki wakavu tena kama awali... Sasa ilikuwa ni wabichi wenye ubora wa kuvuliwa katika siku hiyohiiyo...

Ndoa yao iliukumbatia upweke kwa kila mmoja kuwa mbali na mwenzie... Lakini hakutokea wa kuutamani usaliti... Wakiahidiana na kuimbiana nyimbo moja, nyimbo ya heshima'. Wajiheshimu. Na asitokee hata mmoja wa kuivunja heshima yao.

Kisha, kisha likaibuka tusi jipya huko lilikokuwa... Likasimama katikati yao... Kwa kuwa ni jipya, hawakulijua... Hawakujua...

Loh!

*******

Alizinduka kutoka usingizini kwa kukurupuka. Akawasha taa haraka sana ya pale chumbani.

Akatazama ukutani ili kuangalia muda. Na kabla ya macho yake kutazama saa, yalipishana na picha kubwa iliyokuwa ukutani. Picha ya Bwana harusi na Bibi harusi wakiwa ndani ya tabasamu zito.

Ilikuwa ni picha yao ya siku ya ndoa. Alifarijika kidogo kwa kuwa ilimkumbusha moja ya nyakati bora zaidi katika maisha yake. Kisha akaigeukia saa na kugundua zilishapita dakika kumi tano kutoka kwenye muda sahihi anaopaswa kuamka ili awahi kazini. Akajiandaa harakaharaka na kutoka. Alipaswa kuwahi kuifungua ofisi, ili usambazaji wa samaki ufanyike kwenye mahoteli na 'masupamaketi'. Yeye ndiye mtendaji mkuu. Angetakiwa kuwa wa kwanza kufika zaidi ya mtu yeyote.

Alipoitazama simu yake wakati anatoka, akagundua mkewe alimpigia mara kadhaa na akashindwa kuipokea. Akajikuta akikilaani kitendo cha kuchelewa kulala kisa kutazama mechi ya mpira wa miguu usiku wa jana yake.

Hali hiyo ya kukawia ofisini kwa siku hiyo, ikamlazimu afanye majukumu mengine ambayo hayakuwa yake. Akaingia katika usambazaji kwa kutumia gari yake binafsi. Alifanya hivyo ili kupunguza mizunguko na

kurahisha ufikaji wa oda kwa wakati. Hakutaka kuwakosea wateja wake. Ikiwa ndiyo kanuni yake kuu ya biashara.

Hii haraka yake ikamponza. Akasahau kuwa usambazaji humbatana na ubebaji. Hakuwa ameongozana na kijana wa kwenda kubeba mzigo wakati wa kuutua. Na aliligundua hilo baada ya kuwa tayari ameshafika. Jukumu lote likawa juu ya mabega yake, kwani isingekuwa rahisi kupiga simu na kuita msaada.

Tayari alikwishayaonesha utupu maji, kuyaoga ulikuwa ni wajibu. Alianza kuuburuza kwa kuukokota mzigo huo uliokuwa mzito. Samaki walikuwa wameganda na mabarafu yake. Lakini, katikati ya jitihada hizo, ukatokea msaada. Msaada wa msichana aliyekuwa ndani ya muonekano wa urembo na upole. Bila kusahau roho yake ya huruma. Msichana huyu alivaa sare za eneo hilo. Bila shaka alikuwa ni mfanyakazi wa hapo. Elia alivutiwa mno na ukarimu wa binti yule.

Hata pale kazi ya kuufikisha mzigo ule ilipotamatika akamtolea noti ya shilingi elfu kumi na kumpatia. Ila msichana yule aligoma. Alikataa na kusema amefanya ihsani tu kutoa usaidizi ule. Yule msichana akajazia

hoja yake kuwa lile alilolifanya ni sehemu tu ya tamaduni za kiafrika. Tamaduni za kusaidiana.
Elia alipoona kubembeleza kwake kumegonga mwamba, akaamua kumshukuru kwa kinywa na kuondoka zake. Akiamini jambo lile limeishia pale na halina muendelezo wowote.

*******

Usiku, Elia akiwa amemaliza majukumu yake ya kutwa na kurejea nyumbani. Katika makazi anayoishi peke yake bila msaidizi. Mara chache mkewe huja katika siku za mwisho wa wiki, siku ambazo kwenye kampuni yao binafsi si siku za kazi. Ama yeye kumfuata Mwanza. Lakini kwa siku kama hizo za kawaida, angepokewa na ukimya kama wa usiku huo. Akavua nguo zote na kwenda kuoga. Huko bafuni aliisikia simu yake ikiita, akaamini mpigaji alikuwa ni mkewe.
Akajikalifu kumaliza harakaharaka ili awahi kumpokea. Lakini mpigaji wala hakuwa ni mkewe Tausi. Ilikuwa ni namba ngeni.
Akajisonya kwa ile pupa aliyoifanya kiasi cha kusahau hata kujitoa mapovu masikioni, kisha akaingia zake

moja kwa moja chumbani. Hakutaka kuketi sebuleni tena, aliogopa kujikuta anatekwa na runinga halafu yatokee yaliyotokea usiku uliopita. Aliingia chumbani kwa lengo la kulala. Sikioni ikiwa simu yake, akiipigia ile namba ngeni. Lakini haikupokelewa. Naye hakujisumbua kupiga tena.

Akaingia kwenye majina ili ampigie mkewe...

Mara, ile namba ngeni ikawa inaingia...

Akapokea hapohapo...

"Haloo!" Elia alizungumza.

Upande wa pili ukawa kimya.

"Halooo! Nani?" Ikabidi arudie huku akiuliza.

"Halooow!" Hatimaye ilijibu sauti ya kike katika simu ile. Sauti nyororo.

Elia akajaribu kuikaza ya kwake. "Ndiyo, nani mwenzangu?" aliuliza.

"Naongea na Mr. Elia Maige?" Sauti ya kike ilihoji kwa wasiwasi.

"Mmmh... Ni mimi. Sijui ni nani wewe?" Bado Elia alihitaji kumfahamu yule mpigaji.

"Leo asubuhi ulidondosha kadi yako ya benki, mimi ni yule dada niliyekusaidia mzigo. Sijui unanikumb–"

"Ooooooooowh! Aiseeee!" Elia akamuingilia na kumkatisha. "Daah! Leo umegeuka mkombozi wangu wewe dada! Mungu akubariki sana! Mpaka nikahisi nimeidondosha ofisini. Ahsante sana!"
Yule msichana simuni akawa anacheka, alicheka kisha akasema, "Hamna shida kaka, usijali!"
"Sawa. Kesho nitaipitia basi hapo kazini kwako. Ahsante sana!" Bado Elia aliendelea kushukuru.
Yule msichana naye akazipokea shukurani zile, wakaagana na simu kukatwa.
Baada ya kukata simu, ndipo akili mpya ikamvaa Elia, akili yenye maswali mengi ya kujiumbua..
Sasa mbona sijamuuliza jina?
Kesho nikienda kazini kwake nitamuulizia kama nani na simjui?
Hii namba nitaisevu vipi sasa?
Ngoja nimpigie!
Huo ndo ukawa uamuzi mwingine, akaughairi ule wa kumtafuta mkewe.
Na simu ilipokelewa baada ya kuita kwa sekunde kadhaa...
"Eh! Samahani dada yangu. Sijui imekuaje nimesahau kukuuliza jina lako. Unaitwa nani tafadhali?"

Yule msichana simuni akacheka bila kuongea neno lolote. Cheko fulani hivi la aibu na haya.

"Au nakosea kukuuliza jina lako jamani?" Elia akajishuku.

"Anh! Hapana. Hukosei kaka yangu... Naitwa Suzi!" Msichana akajitambulisha.

"Unait...unasema?" Elia hakusikia vizuri.

"Naitwa Suzi. Suzi Chitete!" Safari hiyo msichana akaipandisha sauti ili asikike kwa urahisi.

Au nawe msomaji bado haujasikia?

Eeeeh!! Anaitwa Suzi!

# 3

"Duniani kungekuwa na watu milioni moja tu kama nyie, tungeishi ka' tuko peponi." Haya yalikuwa ni maneno ya Elia, asubuhi baada ya kumkuta Suzi ofisini. Alistaajabu zaidi kugundua msichana yule mrembo alikuwa sehemu ya mapokezi. Kwa msaada ambao binti huyo alimpa jana yake, haikuwa rahisi kumkisia kuwa ni mtu wa kitengo muhimu kiasi kile. Kitengo cha mapokezi.

Kimoyomoyo, akajikuta akimpongeza mmiliki wa 'supamaketi' ile, kwani mtu aliyemuweka eneo hilo alikuwa ni mtu sahihi mwenye roho ya ukarimu.

Suzi alizifurahia zile sifa na shukurani alizokuwa akimwagiwa na Elia. Wakati huo haikuwa noti ya elfu kumi tena. Wala haikuwa pesa yenye asili ya kitanzania. Zilitoka dola zilizonyooka kimuonekano na thamani. Zilitoka karatasi tatu zenye thamani ya dola kumi kila moja. Jumla dola thelathini. Zaidi ya shilingi elfu sitini kwa pesa za kwetu.

"Utakunywa soda hii!" Elia akamalizia na kumimina tabasamu lililojaa utajiri. Suzi Chitete ni mzoefu wa matabasamu hayo, aliliona na kulihifadhi.

Wakaagana.

Kwa mara nyingine, Elia aliondoka akiamini makutano yale yameishia pale na hayana muendelezo wowote. Akasahau simu yake 'ililisevu' jina la msichana huyo kwa usahihi kabisa, tena kwa herufi kubwa, SUZI CHITETE!

Halafu mie bwana!

Hivi huyu Elia kasahau au kajisahaulisha?

*******

Nyakati za ukumbusho zikawa ni zilezile, usiku.

Baada ya kutoka zake katika kibarua. Siku hiyo aliibadili ratiba yake ambayo mara nyingi aliizoea. Ratiba ya kupita nyumbani kwa rafiki yake, kisha angebadili nguo, hapo wangekwenda kilabuni kupata pombe za kuwasogeza mpaka saa za usiku mkubwa kisha angerudi kwake akalala.

Ratiba yake ya kwenda kazini ilikuwa na mfuatano wa siku tatu, kisha siku tatu nyingine ni za mapumziko.

Haikuwa kazi ya ujira mkubwa, lakini ujanja aliokuwa nao wa kuutumia mtaji wa asili ambao Mungu alimuumba nao, nd'o ulimuwezesha kupanga chumba kizuri maeneo ya mjini. Chumba chenye choo pamoja na bafu kwa ndani.

Alipoingia tu ndani kwake, aliziondosha nguo zote mwilini. Zote, na kubakiwa kama alivyo, akapitiliza kuoga. Kisha akatoka akiwa amejifunga taulo jeupe na kujitupa kitandani.

Akashusha pumzi zake.

Anapenda sana muziki mzuri, laini, wa taratibu, wa kiingereza, akawasha redio yake na kuucheza wimbo wa mwanadada Shania Twain, 'Forever and for always'.

Mashairi yakaanza kuyapepea masikio yake, ingawa hakuyaelewa, lakini alivutiwa nayo kiasi cha kuyafumba machoye. Wimbo ulijaa harufu kamili ya mahaba.

Kwa dakika chache akajikuta akitamani kuwa kwenye mahusiano na mwanaume. Apate mwanaume wa kutulia naye. Aache tabia ya kuhangaika.

Na katikati ya mawazo hayo, ile hifadhi ya tabasamu la Elia ikajifungua rasmi. Tabasamu la hela yote!

Akajibilingisha pale kitandani na makalio yake yakabaki juu, akawa amelalia tumbo na kuifungua simu yake iliyokuwa palepale kitandani. Simu ya bei kubwa. Macho matatu.

Moja kwa moja akaenda kwenye mafaili ya picha, picha zake.

Akaifungua moja ambayo aliyokuwa amevalia kigauni kifupi cheusi kilichokuwa kikiyaweka mnadani mapaja yake meupe. Kinguo hiki kikakomea juu ya kifua kilichokuwa katika ujazo mfano wa vifuu vya nazi zilizogoma kukomaa. Akajikuta akitabasamu mwenyewe kwa namna alivyokuwa ameumbika. Akaikuza ile picha na kuisogeza mpaka ilipo sura... Akayatazama macho yake yenye umbo la samaki, macho ambayo muda wote ni kama yamebeba usingizi yakiwa yamepakwa wanja uliokubali kupakika. Bila kuzisahau papi laini za mdomo ambazo zilibeba rangi nyekundu isiyokuwa kavu...

Mwisho kabisa akaifikia ile pua ambayo ilichongoka kwa wastani na kipini kikining'inia.

"Hapa tunguli ya nini sasa?" Akajisemea huku akicheka.

Akiamini muonekano wake ni silaha muhimu sana ya kumnasa mwanaume yeyote yule amtakaye katika

dunia hii. Akiwa yule ambaye aliingia kwenye rada zake ndani ya siku mbili hizo. Bwana Elia Maige!

Ndiyo! Na kama Bwana Elia bado huko alipokuwa alikuwa akihisi kwamba kitendo cha kukutana na Suzi kilitokea kwa bahati tu, basi angepaswa kuzifuta kabisa hisia hizo. Kisha aketi chini kuelezwa kuwa maana sahihi ya bahati ni maandalizi yaliyokuwa yamekutana na fursa.

Suzi siku zote Suzi huwa amejiandaa. Muda wowote huwa kama simba katika harakati za mawindo yake.

Kwani hata hiyo kadi ambayo Elia aliambiwa ameidondosha, wala haikuwa kweli. Ni Suzi ndiye aliinyofoa kutoka katika mfuko wa mwanaume huyo baada ya kuona ikining'inia. Akiwa na lengo lenye kusudi la kutaka kuanzisha mazoea na mwanaume huyo. Mpango uliokwenda kama alivyotaka.

Sasa ana namba ya Elia Maige kwenye simu yake, mwanaume mwenye uwezo wa kutoa dola thelathini kama shukurani tu ya kuokotewa kadi. Tena akidai ni pesa ya soda.

Huyu akipewa 'popo kanyea anga' si atatoa mpaka viwanja vya makaburi ya babu zake huyu?

Ndivyo Suzi Chitete alivyokuwa akifikiria.

Akajikuta akitamani kumpigia mwanaume huyo. Lakini akasita. Akiwaza na kuhofu namna ambayo Elia angemshtukia lengo lake kwa mapema.

Akaghairi zoezi hilo.

Akamfuta kabisa Elia katika hesabu zake kwa usiku huo.

Kisha akatoka kule kwenye picha na kuingia Whatsapp. Kulijaa jumbe nyingi, na chache sana kati ya hizo zikiwa ni za wanawake. Zilizobaki ni za jinsia isiyo salama kutokana na namna aliumbika.

Hakufungua hata moja, akaenda kwenye uwanja wa 'status', mara, bila kutegemea, anakuta Bwana Elia Maige naye ameweka 'status' muda mchache ambao ulipita. Kama dakika tatu tu.

Haraka sana akazama 'inbox' kwake. Akaingia kikashani mwake na kuona kuwa bado yuko mtandaoni. Kwa lugha iliyo rahisi kwa wengi, yuko 'online'.

"Mmnh! Hulali?" Suzi akatuma ujumbe huo. Zikatokea tiki mbili, lakini hazikubadilika rangi, kuashiria kuwa ujumbe wake haujaonekana. Haujafunguliwa.

Akaendelea kusubiri. Dakika zikasogea. Ujumbe bado ulikuwa vilevile. Haujatazamwa.

Akakwazika. Akazima kabisa mtandao wenyewe kwa kuhisi labda amepotezewa na kuweka simu kando.

Lakini, Suzi bado moyo wake ulikuwa unamuwasha. Ile haikuwa dawa hata kidogo. Aliendelea kumfikiria Elia. Hasa kutokana na ule wimbo wa mahaba ulivyokuwa ukijirudia. Ukamkumbusha kuwa anahitaji kupata mwanaume. Mwanaume wa kumhudumia.

Liwalo na liwe!

Suzi akaamua kuchukua maamuzi. Akakamata tena simu yake. Safari hiyo, akiamua kumpigia kabisa Elia. Alimpigia na asijue atasema nini.

Ni basi tu, ndivyo alivyo, akitaka lake, hugeuka mfamaji...

Heshi kutapatapa!

Simu ikapokelewa. Bila kusalimu, akaanza kuangusha kilio. Suzi alikuwa akilia. Kilio kikali kumzidi mwana mteke aliyepokwa titi na yungali njaani.

# 4

Kama ilivyo ratiba yake ya siku zote, usiku huo Elia akiwa amemaliza kuzifunga hesabu za siku ofisini. Wale wanaolipwa kwa mfumo wa posho za kutwa akawapa stahiki zao za kuhakikisha kila kitu kipo sawa kwa ajili ya kuanza siku mpya iliyokuwa ikifuatia. Ikafuatia safari ya kuelekea nyumbani.

Katikati ya safari hiyo akapokea simu yenye namba ngeni. Simu hii ikimhitaji aingie whatsApp mara moja. Akakubali lakini hakutekeleza.

Akipanga kufanya hivyo mpaka pale ambapo angefika nyumbani.

Kuwasili kwake tu katika nyumba aliyokuwa akiishi, kukafuatiwa na kuishika simu yake na kutazama alichokuwa ametumiwa.

Alitumiwa picha. Akazifungua na kukuta ni picha za mwanaume na mwanamke.

Yule mwanaume hakuwa akimfahamu. Lakini mwanamke alimjua. Ni mkewe. Mkewe Tausi. Mandhari ya picha zile ilikuwa ni maeneo kama baa

hivi, lakini hakutaka kuthibitisha hilo. Akatoka haraka sana na kuipiga ile namba ambayo ilituma picha. Simu haikupokelewa mpaka ilipokata.

Mara ujumbe mpya ukaingia tena. Ni kutoka kwenye ileile namba ambayo punde aliipiga na asipokelewe.

Ujumbe ulisomeka hivi...

THE CASK BAR AND GRILL, JUZI, SAA NNE USIKU.

"The cask? Baa? Mbona hajaniambia?" Alijikuta akijiuliza kwa sauti. Analifahamu vizuri eneo ambalo alitajiwa. Anazijua starehe za eneo hili.

Mkwewe alikuwa anatafuta nini hapo saa nne usiku bila ya taarifa yake?

Tena akiwa na mwanaume!

Akavifungua vifungo vya shati aliyokuwa ameivaa. Hakujua alifanya hivyo kwa joto ama limeanza kumbana kwa kunenepa ghafla, akaketi kwenye kochi. Bado hakuwa ameingia chumbani.

Akaipigia tena ile namba ili apate kuzungumza na yule mtoa taarifa. Ikawa vilevile, simu haijapokelewa.

Yanini aandikie mate na angali wino anao?

Akaona abadili uamuzi na kumpigia mkewe.

Loh! Simu haipatikani.

Akakumbuka kuwa mkewe alimuarifu wakati anatoka ofisini kwamba simu yake inakaribia kuisha chaji, hivyo muda wowote ingezima.

Akachoka!

Akawa ameingia tena mtandaoni kwenda kuitafuta ile namba. Kila alipotuma ujumbe, hakukuwepo na majibu.

Tuma na kutuma... Hakujibiwa.

Mawazo yakaanza kumtafuna. Tabia ya usaliti ni jambo ambalo hakuwahi kuliwaza kama lingekuja lifanyike kwa Tausi. Mwanamke aliyotokea kumuani kuliko maelezo yoyote yaliyowahi kuandikwa ama kutamkwa kuhusu imani. Katikati ya fikra hizo, usiku uliendelea kusogea, usingizi ukampaa, wivu ukazidi kumng'ong'a.

Akachukua simu yake, akaingia WhatsApp na kwenda uwanja wa 'status', akaweka tangazo la biashara yake aliyokuwa akiifanya. Ikiwa ni sehemu ya majukumu wanayofanya kwa ukamilifu. Yeye na mkewe!

Ilipofika hapa kwa 'mkewe', kitu kikali kikamchoma kwenye chembe. Akajikuta anaiweka chini simu yake na kuinuka juu mpaka lilipo jokofu la maji. Lengo amimine anywe.

Ni hapo ndipo alipokumbuka kuwa hakuchukua glasi. Akatoka pale kwa nia ya kuifuata, akajikuta anawasha feni na kuisahau kabisa kuhusu glasi na hayo maji.

Mara aende chumbani avue soksi... Halafu arudi nazo sebuleni kazishika mkononi...

Ama! Kumbe tenga la nguo chafu haliko huku! Anarudi tena ndani!

Harakati hizi zilizokosa mpangilio zikakwaana na muito wa simu yake. Haraka sana akasogea mpaka ilipo akihisi ni mkewe ama yule ambaye alimtumia picha...

Yeyote kati ya hao alikuwa ni wa muhimu kwa nafsi yake kwa wakati huo...

Kufika, mpigaji ni SUZI CHITETE.. Akashusha mabega yake kwa namna alivyokuwa amechoka kwa kukuta kile ambacho hajakitamani. Alihitaji kujua kuhusu zile picha, sio kingine.

Lakini kwa umuhimu aliomfanyia binti huyo, umuhimu wa kumuokotea kadi ya benki na kumrejeshea, akaipokea simu yake.

Ajabu ya Rahmani anasikia kilio!

"Suzi, nini?" aliuliza kwa mshtuko.

Suzi hakunyamaza. Kilio bila neno lolote!

"What's happening Suzi? Tell me!" Akaweka kabisa lugha ya msisitizo.
Suzi haongei. Kilio cha kwikwi!
"Suzi.. uko wapi?" Akauliza swali lingine ambalo liligeuka kitanzi chake. Ama tuseme ndoano kwa usahihi zaidi.

*******

Zilikuwa ni nyakati ambazo Elia angetakiwa kuwa usingizini kwa ajili ya asubuhi ya majukumu ya kiofisi. Lakini simu ya mwanamke aliyekutana naye kwa siku mbili tu, ikamfanya achome mafuta ya gari mpaka mitaa ya Mikocheni. Hakupima wala kuzingatia hatari yoyote kuhusu usalama wake. Sijui ni akili yake ilivurugwa na zile picha za mkewe. Labda. Kwenye hilo tusimlaumu.
Aliuzungusha usukani hadi kwenye namba ya nyumba ambayo alielekezwa. Akaambiwa eneo hilo wapo wapangaji wengi. Hivyo gari yake angepaswa kuipaki nje na kumpigia mlengwa.

Akafanya alivyotakiwa. Na alipofika nje ya geti jeusi, baada ya kuhakikisha ni namba ya nyumba aliyotajiwa, akatoa simu na kumpigia mwenyeji wake. Dakika chache Suzi akatoka akiwa na machozi kedekede mashavuni. Yumkini kuyatazama yale machozi yakamfanya Elia asitilie maanani jinsi msichana yule alivyokuwa amevaa...

Akakaribishwa katika moja ya vyumba vilivyokuwa ndani humo. Mlango ukafungwa.

Nini shida Suzi?

Swali hilo akaliuliza makalio yake yakiwa yapo juu ya kitanda kilichokuwa na shuka jekundu lenye kung'ara. Hakukuwa na kiti ndani humo.

Suzi aliketi kwa pembeni yake. Kainamia. Taulo alilokuwa kalifungia kifuani limayaachia wazi mapaja yake yaliyokosa michirizi.

Achana na huyo Suzi mwenyewe. Mule ndani kulinukia nyie. Sithubutu kukueleza kuhusu ule muziki laini uliokuwa ukisikika kwa mbali.

Suzi akaanza kujieleza. Akiwa kainamia vilevile. Akalalamika mpenzi wake amefariki usiku huo. Mpenzi wa maisha yake.

Oooh! Suzi! Suzi mpenzi yupi Suzi wewe?

Tazama! Elia akamsogelea. Akamshika mgongo na kumbembeleza akiamini anamfariji na kutoa pole zisizo na idadi.

Akaanza kumpapasa huku akimtamkia maneno ya faraja.

Sikia! Mnakumbuka mwanzo niliwaambia tusimlaumu? Kwa hili sasa, mshushieni tu hizo lawama. Ule mpapaso aliouanzisha ulikwenda kuyapandisha maruhani ya Suzi. Binti akajilaza mapajani mwa Elia. Naye akampitishia mkono mgongoni. Mkono wa kushoto. Wa kulia ukabaki palepale mapaji ukisubiri shambulio la mwisho.

Suzi akainua uso wake sasa. Ule weupe wake ulishageuka na kuwa wekundu. Uzuri uligoma kubadilika, ulibaki vilevile. Macho kayalegeza. Yanapanda na kushuka kama kuna vile alikuwepo mtu aliyeyaamuru yafanye hivyo na hayataki.

Nyuso zao zilikuwa mbali kwa sentimita ishirini. Hatimaye zikapungua na kubaki tano tu.

Mwisho kabisa, ikasalia moja...

Moja nayo ikawafuta wenzake walipokimbilia.. hatimaye vinywa vikasalimiana. Ndimi zikafanya

mchakato wa kucheza pamoja... Ndimi zikacheza mieleka..
Pindu pindu! Pindu nikupindue!
Ule mkono wa kulia wa Suzi uliokuwa pale mapajani ukisubiri dakika za majeruhi, muda muafaka ukawa ni huo...
Ukasogea mpaka ilipo hazina kuu ya kiume... Ukafanyika ukaguzi maalumu hapo..
Mapato yakawekwa huku, matumizi kule..
Elia chali!
Ajiweze kwa lipi?
Askari wote wanaojulikana mwilini mwake walishasalimu amri. Wangetii yote ambayo Suzi angesema na kuwaza. Akabaki mmoja tu. Amiri jeshi mkuu. Huyu nd'o muda wake sasa huo. Alikakamaa.
Suzi moyoni akaamini sasa kazi imekwisha. Akajilaza kitandani na kumuacha Elia amfute kwa juu.
Kisha, binti huyu mwingi wa mkole, akalitoa lile taulo lililokuwa mwilini mwake.... Kero zote zikasalia wazi zikimchekea afisa pekee wa utatuzi aliyekuwa zamu kwa wakati huo. Elia.
Hapa sasa siwafundishi...
Mtamlaumu... Mtampongeza...

Ni ninyi na maamuzi yenu...!
Nasemajee, ni ninyi na maamuzi yenu!

# 5

Yalikuwa ni maigizo yanayofanana yaliyofanywa na watu wawili kwa vipindi tofauti. Alianza Suzi.

Punde baada ya safari isiyohitaji chombo kumalizika, akaingia kwenye kilio. Kilio cha chinichini huku akiwa kaufunika uso wake kwa haya. Ikaja zamu ya Elia. Yeye igizo lake lilikuwa ni la kuomba radhi. Kusisitiza kwa binti huyo kwamba eti kile kilichotokea hakukikusudia.

Ilidumu hivyo kwa dakika tano, Suzi akanyamaza huku akifinya finya mafua.

Kiwango bora kabisa cha kuvaa uhalisia alichojaaliwa binti huyu!

Pumzi za Elia nazo zinashuka na kutambua mishale ya saa ilikuwa ikiitafuta saa sita.

Muda wa kuondoka!

Mwanaume huyu akajikusanya na kuitafuta shati alipoirusha.... Suruali nd'o akaipata baada ya kuangalia uvunguni...

Aondoke hivihivi?

Hapana! Akaacha mzigo akidai ni pole ya msiba. Kibunda cha shilingi laki mbili na nusu za kitanzania.
"Anything... Call me! Okay?" Akasisitiza kupigiwa ikiwa kungejiri la kutatiza. Suzi kwa mapozi huku akitazama chini, akaitikia. Aliitikia akiwa palepale kwenye kitanda amejikunyata. Madai yu huzunini.
Elia akatoka kwa hatua za kishababi na kuufunga mlango wa chumba kile. Ukawa mwisho wa maigizo na wote kuingia kwenye ulimwengu halisi sasa!

*******

Akiwa ndani ya gari lake, kabla hajauzungusha ufunguo kuiwasha ili aondoke, aliitoa simu yake na kuitazama. Akakuta imepigwa na mkewe zaidi ya mara tano na isipokelewe.
Mwanzoni, alipotumiwa zile picha, alikuwa amemuhifadhi mwanamke huyo katika mkoba wa usaliti. Lakini kwa tukio alilotoka kulifanya yeye dakika chache zilizopita, hakutamani hata kumpigia....
Kila alipoinamisha pua zake na kujinusa, aliamini ananuka jasho la kukiuka ahadi alizozitoa mbele ya kanisa siku ya ndoa yao.

"Ooh Shit!" Akagonga usukani wa gari lake na kuwasha kiyoyozi baada ya kuvipandisha vioo. "Why! Why! Why Elia? Why? Umefanya nini Elia? Tazama ulivyojidhalilisha! Tazama!" Alijilaumu. "Shiit!!!" Akagonga tena usukani kwa hasira!

Kisha akawasha gari na kuondoka huku moyo wake ukimtetemka. Mtetemeko wa hatia ya kuivunjia heshima ndoa yake.

Kwa Suzi ikawa ni kinyume kabisa!

Kile kilio kilipoyeyukia alijua yeye.

Kwanza ni cha kweli sasa?

Muda huo alikuwa akirukaruka. Akamaliza na kwenda kuoga. Akarudi kitandani na kubadili shuka.

Akawasha feni na kujitupa tena kitandani kuutafuta sasa usingizi huku uso wake ukiwa umechanua tabasamu. Moyoni akijipongeza kwa kazi ambayo aliamini nd'o kwanza imeanza. Mwanzo wenye mafanikio.

Zikapepea siku nne bila ya mfiwa wala mtoa pole kumtafuta mwenzake. Ikiwa ni siku ya Jumapili. Elia hakumuuliza tena mkewe kuhusu zile picha. Akiimaliza kesi hiyo juu kwa juu kwa madai kuwa ni kafara ya dhambi ya uzinifu anayojutia kuifanya.

Jumapili ni siku ya ibada. Alikwenda kanisani kwenye misa ya pili. Lengo, baada ya kutoka hapo, apitilize kwenye kikao cha harusi ya rafiki yake. Ambaye walisoma pamoja chuo kikuu cha Dar Es Salaam. Kikao kilichokuwa kikifanyika nyakati za jioni.

Elia yeye ni muumini wa kanisa maarufu mjini humo, kanisa la Ufufuo na uzima, lililopo maeneo ya Ubungo. Alipomaliza ibada, alinyoosha moja kwa moja Mbezi. Huko ndiko kikao hicho kilipangwa kufanyika. Nyumbani kwa rafiki yake. Kufika mahala. Ikiwa ni njiapanda. Akawa amesahau kama aliambiwa akunje kushoto ama aelekee kulia... Akatoa simu ampigie mwenyeji.

'Ndugu mteja, salio la kwenye simu yako, halitoshi kupiga...'

Akakata! Akasonya!

Akasonya tena baada ya kukumbuka kuwa hata kwenye akaunti zake za mtandao hakukuwa na akiba yoyote ya shilingi. Pesa zote alizitoa. Akapaki pembeni gari yake. Na alipoyapepesa macho yake kuangaza kwa pande zilizo na idadi iliyomkifu, akakwaana na kibanda kilichopambwa kwa neno kubwa. WAKALA.

Akaziwahisha pua zake hapo. Macho yake yakiwa yameganda kwenye simu yake kutazama muda, ambao kimsingi tayari ulibeba sura ya yeye kukawia kwenye kikao. Lakini hizi haraka zake zilikutana na mwamba wa mteja mwingine ambaye alikuwa ndani ya mzozo na mtoa huduma.

"Hebu acha maneno makali dada yangu! Sipendi hivyo unavyosema na kuniita mwizi. Mimi nikuibie elfu hamsini inipeleke wapi?" Huyo ni wakala aliyekuwa akijitetea. Elia alimsikia lakini hakumuona. Alizibwa na mteja aliyekuwa akihudumiwa. Mteja wa kike.

"Sasa kama sio mwizi si unipe hela yangu. Mimi natoa hela, unasema sijatoa! Nikueleweje?"

Elia alihisi ni kama vile sauti ya msichana aliyekuwa akilalamika amewahi kuisikia mahala. Ama anaifahamu. Alipoinua uso wake kuutazama mgongo. Ambao kwa chini ulipokelewa na ujazo sahihi wa nyama uliokuwa ukilazimisha kujitokeza nje ya kanguo kafupi alikokuwa amekivaa.

"Kwani hujaona jina hapo? Jina ni Suzi Chitete! Mbona muamala kwangu umeshathibitishwa?"

Elia alishaanza kupiga hatua mbili kuondoka. Akasimama. Kama hilo jina ambalo lilitajawa halikuwa

bado halijatokea simuni mwa wakala, basi kwa mwanaume huyo lilitosha kabisa kumfanya asamehe yote na arudi pale ambapo alitoka.

"Suzi!" Elia aliita.

Msichana akageuka.

# 6

Walipotazamana, ni Suzi. Baada ya kumpa kisogo kwa siku nne mfululizo, hatimaye Elia alimtia machoni binti huyo mwenye muonekano timilifu wa urembo.

"Elia, unafanya nini huku kwa bibi yangu?" Ilikuwa ni sauti laini ya Suzi ikiuliza, huku akiufinya mdomo wake wa chini kwa meno yake ya juu.

"Wow! Ni kwa bibi huku?" Elia akadhihirisha ushtukaji wake, akitazama kulia na kushoto kama vile hiyo nyumba ya bibi aliambiwa imejengwa pale katikati ya barabara.

Walioneshana bashasha, wote kwa pamoja wakijitahidi kuudhihirisha uongo kuwa wamefurahi kuonana. Lakini haikuwa hivyo. Kila mmoja hakupenda kukutana na mwenzake kwa namna ile. Elia akiamini huyo binti mpole aliye mbele yake, ameshamtafsiri yeye ni kama muhuni tu, mwenye maisha ya dondola. Kudonoa na kuondoka. Suzi naye akajipa hatia ya kutomtafuta mtu ambaye alijitoa na kumpa pesa nyingi, kisha asimpigie simu hata ya kusema ahsante.

"Eenh! Ni hapo tu mbele, unaingia kulia, unakunja chini... Umefika!" Suzi akaelekeza, Elia akatikisa kichwa kuitikia kuwa ameelewa. Na angetokea wa kumgonga kwenzi pale akamuuliza huko chini alikoambiwa akunje ni wapi... Asingepata jibu zaidi ya kukuna kichwa chake... Iwe kwa maumivu ama kutafakari, hilo angejua yeye.

"Sasa, mimi naenda kwenye kikao. Ni mitaa hii hii, kinaisha baada ya lisaa. Nadhani sitakaa. Sijui nitakukuta?"

Suzi akatabasamu na kujibu, "Sawa."

Elia akaaga na kuondoka.

Amaa! Si alikuja kwa wakala huyu?

Hilo alikwenda kulikumbuka alivyoingia ndani ya gari na kuliwasha... alipotambua kuwa bado yuko katikati ya njia mbili za kulia na kushoto...

Akashuka tena na kurudi kibandani. Suzi alishaondoka. Akapata huduma na kumpigia mwenyeji.

Safari ikaendelea, moyoni mwake akimshukuru Mungu kwa kumkutanisha tena na Suzi. Akiamini pengine ingekuwa ni nafasi nyingine ya kuomba radhi kutokana na ukatili aliomfanyia. Ukatili wa kumshawishi wakatenda uchafu hali ya kuwa kifua cha

binti huyo kilikuwa kimebeba majonzi ya kufiwa na mpenziwe.

*******

Baada ya kutua uwanja wa ndege wa kimataifa wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, mwanamke mweusi, mnene, ambaye kwa mbali kifua chake kikubwa kilifuatiwa na kitambi, akiwa ndani ya mavazi yenye kuishabihi vilivyo hali yake nzuri ya kiuchumi, alielekea moja kwa moja kwenye taksi mojawapo na kuingia baada ya kuongea na dereva, akasema alipokuwa akihitaji kupelekwa.

Mara kadhaa akiwa njiani, akajaribu kumpigia mumewe na asimpate. Alifanya hivyo kwa lengo la kumuarifu juu ya ile safari ya ghafla ambayo aliifanya bila kumtaarifu.

Lakini hiyo ilikuwa ni Jumapili. Alijua kuwa ni siku ya mapumziko kwa mumewe. Akajitoa wasiwasi kuwa angemkuta tu nyumbani na hakuna ambacho kingeharibika.

Tatizo sugu la simu yake likawa limeshika hatamu. Tatizo la kuisha chaji. Ikazima.

Hakuwa na wasiwasi, alikuwa anakwenda kwake, angeichaji huko.
Ndiyo! Nyumbani kwa mume wake halali wa ndoa ni nyumbani kwake pia!
Hata pale alipofika na kukuta nyumba imefungwa, aliifungua tu kwa funguo nyingine alizonazo na kuingia.
Umaridadi wa mazingira mule ndani haukumridhisha, akakunja ndita zake kadiri alivyokuwa akitazama namna nyumba hiyo ilivyoonesha kutokufanyiwa usafi wa kutosha...
"Elia naye!" Akalalama, kisha akalivaa jukumu la kuinadhifisha sebule, vyumba vikifuatia.

**********

Saa moja ikapita kama inakimbizwa. Simu ya Suzi ikaita. Mpigaji akiwa ni yuleyule mwanaume aliyekuwa akimsubiri. Elia. Kikao kilikuwa kimeshakwisha. Wakapatana pa kukutana. Palepale kwa wakala. Gari ikasimamishwa hapo na mlango wa mbele kufunguliwa. Akaingia Suzi Chitete akiwa amekusanya tabasamu zito wajihini mwake.

"Nimechelewa sana?" Elia akahoji naye akijitahidi kukenua.
Suzi akapeleka kichwa kulia na kushoto. Kwa maringo. Bila kutamka lolote. Jicho lake chovu likitua moja kwa kwa Elia. Akijitahidi kumlaza mtegoni mwanaume huyo kwa mara nyingine.
"Tukakae wapi tuzungumze?" Elia aliuliza.
"Kwani hapa tulipo tumesimama?" Suzi akaleta utani huku lile tabasamu likikomaa na kuwa kicheko. Kicheko hafifu, cha haya...akaziba na uso wake kama vile kule kucheka ni dhambi ya mtu kufanya kwa uficho.
Yote haya Elia aliyatazama. Lakini akazuga kutoyaona. Ipo tofauti kubwa sana kati ya kuona na kutazama.
Akiwa haelewi aanzie wapi kwa lile ambalo alikusudia kuongea, simu yake inaingia ujumbe. Uliomuarifu kuwa kuna namba ilimtafuta na haikumpata. Alipoiangalia, ni namba ya mkewe. Mkewe Tausi. Akakumbuka kwamba aliizima alipokuwa kikaoni kuepusha usumbufu.
Hakumpigia. Akijipa ahadi kuwa angempigia atakapofika nyumbani.

"Enhee! Unase.." akakwama. Kauli haikuisha baada ya kumgeukia Suzi. Binti huyo, lile gauni lake fupi lilishaamua kuyabakiza wazi mapaja yake. Hapa sasa aliona. Hakutazama.

Huyo mwenye maungo yake yupo sasa?

Madai haoni. Kwamba ametingwa na simu yake ya mkononi.

Kisha, mdomo wa Elia ukiwa umeachama kwa uchu wenye kukaribia kumtoa ute, hapo Suzi akajifanya mwenye kushtuka eti. Akalishusha lile gauni harakaharaka na kuomba radhi.

"Usijali. Tunaweza kwenda kuzungumza kwangu?" Elia akaweka pendekezo lenye ukomo wa kusalimu amri. Alishakubali yeshe. Kama kuna lolote basi likajadiliwe nyumbani...

Ndivyo alivyohitaji.

Suzi afanye nini?

Sasa hivi kichwa kikapelekwa juu, kisha chini. Vilevile, bila kunena lolote. Akiamini kama ilivyokuwa kwa jaribio lake la mwanzo, na pili pia limo katika njia salama ya mafanikio.

Wapi?

# Nyumbani!

# 7

SIJUI ni ule upweke! Ila ndo angeshindwa kuwasha walau runinga kubwa iliyokuwepo mule ndani impigie kelele?
Ama ni lile giza lililokuwa linakaribiwa kuingia?, lakini pa kuwashia taa si palikuwa wazi kabisa panaonekana? Ni nini sasa? Ni nini kilichomsukuma ashike simu yake, aiwashe, ampigie mumewe. Elia akaipokea simu ya Tausi akijitahidi kuyaficha mazungumzo yake ili yule binti mule ndani ya gari asihisi chochote... Kwamba alijiuma uma kuongea na mkewe, akilazimisha Suzi asielewe.
Alikuwa akimfundisha mtoto wa chekechea hesabu za kujumlisha, huku akitegemea mwanafuzi wa chuo kikuu aliyekuwa pembeni yake asingeelewa!
"Umeoa?" Swali la moja kwa moja kutoka kwa Suzi akimtazama Elia machoni bila ya kupepesa. Baada ya kumaliza mazungumzo na kukata simu.

Elia akajichekesha. Akiweka koo lake na kujaribu kuzipanga sentensi zake kwenye kujieleza.
Kabla hajafanikisha kuiweka hata herufi moja mahala pake, Suzi alishusha swali lingine, "Sasa kunificha unaona ingesaidia nini?" Alikuja juu.
"Nishushe hapo!" Suzi akaomba gari isimamishwe.
Sasa kile kicheko cha Elia kilipoa na kuhamia kwenye pembe za mashavu, yakawa yanatikisika katikati ya fundo la aibu. Akasimamisha gari na kumgeukia Suzi.
"Naomba nisikilize!" Akaongea kwa mara ya kwanza.
Sio kumsikiliza tu, Suzi hata kumpa uso wake hakutaka. Alikuwa akihangaika kuufungua ule mlango wa kiti alichokuwa amekaa ili atoke.
"Subiri, sijatoa lock!" Elia alinena kwa utaratibu huku macho yake yakitazama yale mapaja ya Suzi yaliyokuwa yatikisika kwa zile hekaheka. Kinguo chake kikiwa kimeshapanda juu zamani sana. Akameza mate ya uchu na kujitetea, "Suzi, huyu ni mama yangu! Amekuja nyumbani!"
"N'fungulie nitoke...please! Nakuomba we' baba!" Sasa sauti ya Suzi ilijaa kitetemeshi.
Cha hasira? Cha huzuni? Haikuwa habari kwa wakati huo zaidi ya yeye kutaka atoke.

Elia akashusha pumzi kwa nguvu. Kisha akaingiza mkono mfukoni na kutoa noti nne za elfu kumi.
"Okay... Utafanya nauli hii!"
Suzi akazitazamaaa, kisha akamuangalia Elia usoni, akasonya kwa nguvu, "Unan'nunua? Unan'chukulia mi' malaya, si ndiyo?" Bado Suzi alikuwa juu na hakutaka kushuka.
Honi zilishaanza kupigwa na gari nyingine zilizokuwa zikija nyuma yao. Hawakuwa wamesimama kwenye barabara kubwa, lakini ilikuwa ni katikati ya njia yenye kutumika na usafiri wa wengi.
Elia akajikuta amekata tamaa, akamfungulia, Suzi akatoka na kuubamiza mlango kwa nguvu. Akabaki mwenyewe ndani ya gari, labda na zile siti ambazo zilikuwa ndo mashuhuda pekee wa tukio lile fupi, ambazo wakati huo aliziona kama zenye kumzomea. Akaiondoa gari kwa hasira. Kituo kikawa nyumbani. Kwa mkewe. Salamu ikamtoka huku kaukunja uso wake.
"Vipi mume wangu, kwema?" Tausi akamuuliza kwa utaratibu baada ya kuona bashasha alilokuwa akilitoa linakosa ushirikiano.

"Kwanini umekuja bila ya taarifa?" Elia anafoka. Tausi anashangaa namna mumewe alivyokuwa wa tofauti. Kwamba leo anagomba amekuja ghafla, ilihali kwa siku za kabla ya hapo alitamani hata mwanamke huyo ahamie Dar Es Salaam.

Akataka ajieleze, "Mume wangu, ni..."

Kabla hajamaliza, "Hakuna cha mume wangu Tausi!" Elia alimuingilia huku akionesha kutotaka maelezo. Kisha akaingia ndani na kuufunga mlango.

Ana nini?

Tausi alisimama peke yake akijiuliza na asijue la kufanya. Akaufunga ule mlango wa sebule na kumfuata mumewe chumbani, alimkuta ameketi katika kitanda.

Au ni changamoto za kazi?

Akajiuliza kichwani. Lakini hilo la changamoto la kazi alijijibu mwenyewe na kujithibitishia lisingekuwepo. Kwani ni biashara waliyokuwa wakiifanya kwa ushirikiano. Alifahamu vema namna ilivyokuwa ikijongea. Hakukuwa na changamoto yoyote.

Ni nini sasa kilichomvuruga?

Bado Tausi aliendelea kujiuliza huku akiogopa kutamka neno. Hakuwahi kumuona mumewe kwenye hasira zile. Hata kwa mtu mwingine.

Akajisogeza karibu yake, akampelekea mkono amshike, aliujua udhaifu wa Elia... Udhaifu wa kuguswa. Akalifanya hilo kwa usahihi kabisa huku ulimi wake ukifanya kazi ya kike, kutamka maneno laini ya kumuingiza mume wake ndani ya kumi na nane zake, ndani ya upenyo huo, akijaribu kumueleza sababu ya yeye kuja kwa kushtukiza, kuwa kuna nyaraka za haraka zinazotakiwa kufuatiliwa kwenye ofisi za mamlaka ya mapato huku mjini, nyaraka hizo zinapaswa zitiwe sahihi zao wote wawili, yeye na Elia.

Wakaelewana. Wakachekeana.

Kifuate nini?

Wakakumbatiana, wakalazana. Wakalaliana...

Nini kingine?

*******

Moja kwa moja alikwenda nyumbani kwa rafiki yake. Bila kauli nyingi baada ya salamu akakamata kilevi na

kugida mafunda ya kutosha. Kidogo ndo akapata nguvu ya kuzungumza.

"Wanaume ni wapuuzi!" Kisha akajilaza chali akimwacha shoga yake aitwaye Lucy kwenye mshangao wenye fumbo kubwa.

"Vipi, umekopwa?" Lucy akakiachia kicheko kilisindikize swali lake.

Suzi hakujibu chochote huku akiwa vilevile katika mlalo wa kulikodolea dari.

"Mnh," Lucy akaguna huku akamwacha Suzi palepale kitandani na kutoka zake nje.

Suzi alikuwa kwenye hisia ambazo kwa kipindi kirefu hakupishana nazo maishani. Kuna kitu kilikuwa kikiutoboa uvungu wa moyo wake kadiri alivyokuwa akiikumbuka simu ya Elia na namna alivyokuwa akizungumza, kilizidi kumtia maumivu.

Suzi alijikuta ndani ya wivu wa kisicho halali kwake.

# 8

Imetamkika kuwa, wanandoa hugombana kuanzia kwenye kitovu kuja juu tu. Na hata kupatana kwao, huanzia hapohapo kwenye kitovu, kuja chini!

Elia na Tausi walikuwa juu ya kitanda, Tausi kakilalia kifua cha mumewe akimtaka radhi. Kinywa cha Tausi kilijaa utulivu katika kujikomba, lakini moyo wake ulikuwa kwenye mateso makubwa ya kulitafakari jambo. Kuna swali lilikuwa likikizonga kichwa chake kutokana na jambo jipya alilokuwa ametoka kulishuhudia muda mchache uliopita kwa mumewe. Haikuwa ile hasira ambayo Elia alirudi nayo nyumbani hapo, kipo kitu kingine kilichokuwa kikimtanza Tausi. Mumewe alibadilika. Alikuwa akiuwaza ufanisi wake mdogo kwenye tendo.

Huyo si Elia ambaye Tausi alikuwa akimfahamu.

Elia wa dakika tano awe hoi?

Hapana! Kuna mahala tu penye tundu palipokuwa pakivujisha penzi lao. Ndivyo Tausi alivyokuwa akihisi na alihitaji kuupata uhakika. Ile lugha laini aliyokuwa

akiitumia pale kwenye kitanda huku akikipapasa kidevu cha mwanaume wake, ilikuwa ni sehemu pana ya mbinu ambayo aliifanya kwa kukusudia Elia apitiwe na usingizi ili akaichukue simu yake. Alihitaji kuipata simu ya Elia kujua kitu gani kilichokuwa kikijiri nyuma ya pazia. Kuhakikisha hilo linatimia, akajaza na shinikizo kwenye maneno yake...

"...Pumzika, nataka mpaka ukiamka, chakula kiwe kimeiva. Sawa mpenzi?"

Jitihada zikazaa matunda. Koo la Elia lilianza kutoka radi zenye miungurumo kuashiria kuwa mvua ya usingizi imeshika hatamu.

Mwanamke huyu mnene akajiinua kwa wepesi wa puto ili asisikike, anakaelekea kwa hatua za paka mpaka ilipo meza. Akaikamata simu. Akazima na taa taaratibu kabisa. Taa ya kile chumba. Kisha akatoka nje.

Moja kwa moja jikoni. Huko, hakukamata sufuria wala mwiko...

Aliketi chini, na kuanza kuipekua. Moja kwa moja eneo la ujumbe. Juu kabisa, wala si popote, juu... Jina likajitokeza...

SUZI CHITETE!

Akalifungua baada ya kuguna.

Yalikuwa ni mazungumzo ya jioni hiyohiyo. Yakimuonesha mume wake kuna msichana aliyekuwa akihitaji kuonana naye na walipanga kukutana. Mazungumzo hayo hayakuwa na uthibitisho zaidi. Kwani yalionekana ni ya kawaida na kukosa vitu vizito vya kushibisha kuwa kuna baya lemye kuendelea kati yao. Akatoka na kutafuta jumbe nyingine, ambazo kwa wingi wake zilibeba tarehe za siku tatu mpaka nne nyuma. Akaachana nazo. Akarudi kwenye jina Suzi na kutazama vizuri, ni kama hakuridhika au aliamini macho yake awali yalimuongopea. Alipothibitisha kile alichokuwa akikitazama ni kilekile cha awali. Akasonya kwa nguvu huku akiitupa simu kando...

Mpaka hapo chui anayenyemelea zizi lake alimhesabu kuwa ni Suzi. Akaikusanya nia kwenye kifua chake, akisubiria pale ambapo mumewe angeamka, swali lingekuwa moja tu...

Suzi ni nani?

Kisha akabandika maji kwa ajili ya kusonga ugali. Muda ulikwenda sana, aliona mlo huo ungekuwa ni wa haraka zaidi, na vile katika jokofu kulikuwa kuna samaki, angewakaanga na kuwakatia kachumbari.

Chakula kitamu, chenye kuhitaji maandalizi ya muda mfupi.

Muda!

Muda wa kusubiri yale maji yachemke, kichwa chake kilizongwa na jina Suzi. Akajikuta anaitamani upya simu ya Elia huku shabaha yake ya awamu hiyo ikiwa imebadili uelekeo. Alienda eneo la picha. Akaanza upekuzi mpya hapo. Picha ya kwanza... Pili... Tatu..

Ana kwa ana na mwanamke anayefanana na yeye, akiwa na mwanaume pembeni...

Akapikicha macho yake vizuri kutazama.

Ama! Huyo mwanamke ni yeye na mwanaume wa pembeni pia alikuwa akimtambua. Yale mapigo ya moyo yaliyokuwa yakimwenda kasi kwa hatua mbilimbili kifuani mwake shauri ya wivu, sasa yalikuwa yakizochota hatua nne kwa mpigo shauri ya hofu!

*******

Muda huohuo, baada ya zimwi la wivu kumyeyuka, zimwi asilofahamu ubini wake wala lilipotokea, Suzi alijivuta na kuketi kitandani. Aliingia mitandaoni, kwa kuanza na WhatsApp. Huko akakutana na utitiri wa

'meseji' kutoka kwa wanaume tofauti. Huyu akilalamika kwanini hajibiwi, mwingine akiulizia ikiwa hela aliyotuma imepatikana, wale waliosalia wakifanya maombi ya kukubaliwa hitajio lao la mahusiano. Mtandao huo ukawa kero ya kumchefua, akatoka na kuhamia Instagram. Ambapo aliperuzi kwa dakika chache na kuzitazama picha zake za nusu utupu namna zilipokea maoni na wingi wa kupendwa. Tabasamu hafifu likamchanua katika papi zake laini za mdomo ambao kwa hakika kuna upendeleo ulifanyika wakati wa uumbwaji wake. Mara, akakwaana na picha nyingine. Hii haikuwa yake, bali ya mwanamke kama yeye, pembeni ya mwanamke huyo, kulikuwepo mwanaume mwenye muonekano kamili wa pesa. Mate ya uchu yakaliparaza koo lake. Ni katika nukta hiyo jina Elia ndipo liliporudi upya katika utawala wa kichwa chake. Alihitaji maisha ya mwanaume... Mzuri... Mwenye hela... Na kila alipopepesa kope zake, Elia ndiye aliyekuwa akimjia kwa mbele.

Nafsi ikamsuta kuwa Elia ameoa na ana mke wake. Kisha, nafsi hiyohiyo ikawa kigeugeu na kumtilia walakini kuwa pengine yale aliyoelezwa kule kwenye gari ni kweli. Yumkini yule aliyekuwa akiongea kwenye

simu ni mama yake. Akajikuta mwenye hatia namna ya alivyomjibu na kukosa usikivu. Suzi akahitaji aombe radhi.

Simu iko wapi?

Akaichukua. Akili ya kupiga ilimjia, lakini akaipuuza kwa kuona isingekuwa namna sahihi, kwani, labda muda huo Elia angekuwa kwenye mazungumzo na mzazi wake. Akaingia kwenye ulingo wa ujumbe.

'Samahani, ni hasira tu'. Mwanzoni aliandika maneno hayo. Kisha akanyanyua macho yake darini kutafakari. Akaona ni maneno magumu sana. Akayalainisha kidogo kwa kuongeza kiungo cha lugha kuuongeza utamu...

'Baby, am sorry... Ni hasira tu!'.

Huo sasa hata alipoutazama yeye kabla ya kuutuma, ulimridhisha. Akafanya alichodhamiria bila kujua ya bomu alilokuwa akilisuka ni kubwa kiasi gani na hakuwepo kiumbe yeyote duniani wa kulitegua.

Achana na binadamu...

Nimekwambia kiumbe yeyote!

# 9

Yalikuwa ni marudio ya kitendo kimoja chenye kufanywa na vidole viwili vya mkono wa kulia: kidole gumba na kile cha shahada. Aliikuza picha na kuifanya ndogo. Kila alipokuwa akitafakari ni kwa pembe ipi picha hiyo ilinaswa hakuna jibu alililoweza kulipokea.
Bado moyo wa Tausi uliendelea kuicheza ngoma iliyokosa mdundo wenye utulivu. Picha ilionekana kuwa ya muda mrefu katika simu.
Taratibu, akaanza kuhisi kule kubadilika kwa Elia huenda kumesababishwa na jambo hilo. Tausi akashusha pumzi.
Atasema nini aeleweke?
Aliwaza.
Ubongo wake ukakiri kuwa hauna uwezo wa kumpa jibu zaidi ya kufikiria namna mwanaume huyo angeanza kulalamika. Anamfahamu mumewe, si mtu wa kufoka. Lakini anapoanza kuziteremsha lawama,

unaweza kumuomba akupiga kofi la uso udondoke na uzimie. Uje kuzinduka hasira zimemwisha.
Akaiweka ile simu chini. Hajanyanyua mkono wake, simu ikalipua taarifa ya ujumbe. Moyo wake uliokosa hamu ya kufanya lolote ukamshawishi aiache. Akautii.
Akaketi chini na kukishika kichwa chake chenye nywele ndefu za kusokotwa. Alitamani azinyofoe. Kuna namna alikuwa akihisi zikiuongezea uzito utosi wake. Kisha akainuka juu. Akaelekea chumbani kwa kujivuta. Sala zake zikiwa nyingi. Huku sentensi zote zikikosa neno Mungu na kutawaliwa na jina Elia.
'Naomba Elia wangu anisamehe!'
'Naomba Elia wangu asibebe hasira kali na anisikilize!'
Moyo wake uligeuka kanisa la kujitegemea ndani ya muda mfupi.
Alipoufungua mlango, sauti ya mtu akoromaye ikamlaki. Elia bado alikuwa usingizini.
Akaokota fikra ambazo alizikaribisha kama tunu ya ukombozi. Yeye aliamini ni za kumsaidia. Alipata mawazo ya kuirejesha simu kitandani na kuigiza hakuna chochote alichokigundua wala kukiona.

Hatua za harakaharaka zikamfikisha mbele ya kuta za jiko, mguu funika, mguu funua, simu hii hapa mbele yake!

Akaikamata. Akajisemea afungue ili kufuta ushahidi wa lolote, pale ambapo Elia angekuja kuigusa, na asigundue kama simu yake ilipekuliwa.

Jina suzi likapepea mbele ya mboni zake. Likapepea kwa madoido na dharau juu. Likithubutu kumuita mumewe kipenzi 'Baby'.

Mwili wa Tausi uliokuwa katika joto kali, ukazama katika baridi zito ndani ya sekunde chache. Aliutazama ule ujumbe mara mbilimbili.

Kila alipoyafunga macho yake, koo lake likapitisha mate ya uchungu. Uchungu wa kusalitiwa.

Kifo cha mende, ndege kaning'inia tawini, mbuzi kagoma kwenda, msaada tutani, nyama-ubavu, sitini na tisa.. mitindo yote ya ngono kitandani ilianza kujichora katika neva za fahamu zake, akaanza kupata picha halisi namna mumewe alivyommiminia mahaba mwanamke wa kuitwa Suzi hata kufikia kumuita 'Baby'!

Nafsi yenye kutapatapa ikamkosesha subira na uvumilivu. Akaingia katika ulimwengu wa maamuzi na kumpigia Suzi.

Simu iliita. Ndani ya sekunde tatu ikapokelewa.
"Halloow!" Ilizungumza sauti ya kike iliyojaa utulivu upande wa pili wa simu.
"Hellow! Elly?" Sauti ikajitamkisha tena. Labda baada ya kuona ukimya umetawala.
Ni hapo ndipo Tausi aligundua mumewe sio 'Baby' tu, kumbe jina lake linaweza kukatishwa na likavutia kupitiliza.
Akazikusanya nguvu chache zilizokuwa zimesalia ndani ya kifua chake, huku nyingi zikiwa zimeshasombwa na mawimbi ya wivu. Akajitahidi kujieleza akihisi kama kuna mbanano mkali wa pumzi kifuani mwake , "Mimi, mimi naitwa Tausi. Mke wa Eli–"
Hajamaliza, simu ikakatwa.
Tausi akaona amempata mwizi wake na keshamzamisha katika kumi na nane. Akapiga tena simu na kuiweka sikioni.
Ikapokelewa.
"Naongea na nani?" Sasa alipata ujasiri wa kuhoji.
"Suzi!" Upande wa pili ukajibu bila kuonesha hofu ya lolote.
Tausi akarudia maelezo ambayo aliyatoa awali, "Mimi ni mke wa Elia!"

"Nilikusikia vizuri dada. Nikusaidie nini?" Bado Suzi alikuwa ndani ya utulivu uleule.

"Nikuulize wewe. Nikusaidie nini? Mbona unamuita mume wangu majina ya ajabu?" Mwanamke wa kisukuma akaingia ndani ya kufoka.

"Mume wako au mume wetu dada? Mbona unajimilikisha sana?" Miondoko ya Suzi ilikuwa juu ya mstari uleule wa kujiamini.

"Mume wetu? Mshenzi wewe! Unapata ujasiri wa kusema hivyo kama nani?" Tausi alizima moto wa chakula kilichokuwa jikoni. Samaki walianza kutoa kelele ya harufu kuwa wameiva na sasa wanaelekea kuungua.

"Dada, naomba maelezo mengine umtafute mumeo, umuulize. Lakini mimi hapa unayenisikia, ni mke mwenzako!" Kauli ya mwisho, simu ikakatwa.

Jaribio la marudio la Tausi kuipiga tena likagonga mwamba. Hakupokelewa.

Mashavu yakamtutumka. Machozi yakamlenga. Kila alipoitazama ile simu, alitamani imtengenezee mlango kwenye uwazi wowote ili ajitose amfuate huyo mwanamke bazazi wa mapenzi. Suzi.

Katikati ya fukuto hilo, mnuko wa manukato ya mumewe ukasogeka mpaka kwenye mlango wa kuingilia jikoni. Alipoyainua macho yake, yalikutana na tabasamu.

Kwa mara ya kwanza tangu walipofunga ndoa yao, akajikuta akilichukua tabasamu la mume wake. Alimtazama kwa jicho kali.

"Kuna nini mke wangu kipenzi? Uko sawa?" Kauli ya kinafiki ikapenya katika tundu za masikio yake, humo, ikabeba tafsiri nyingine, ya 'Unanuna nini mke wangu mshenzi?'

Hakumjibu. Akamsonya kwa nguvu na kwenda kumvaa pale katikati ya mlango alipokuwa amesimama. Akamzoa kwa kikumbo na kumuweka kando. Mwili wa Tausi ulikuwa mkubwa zaidi ya ule wa mume wake. Ulitosha kumpepesua na kukaribia kumdondosha chini. Alipofika mbele, akasimama. Bado Elia alikuwa haelewi chanzo cha varangati lile. Tausi akarudi nyuma na kumkabidhi simu yake.

"Kuanzia leo mke wako ni Suzi!" Alimaliza kwa kulimwaga zigo la roho, akaelekea chumbani. Hakwenda kulala ama kulia kama ambavyo Elia

alikuwa akifikiria. Alidhamiria kufungasha mizigo yake. Aondoke. Usiku uleule.

# 10

'TAUSI ameshika simu yangu. Amempigia Suzi na wameongea mengi...'
Haraka sana sentensi hizo mbili zikaweka nanga ya muda mfupi katika fikra za Elia. Na alipoifungua simu yake, akaona rekodi ya Suzi kupigiwa ndani ya dakika chache zilizopita.
Hakuweza kujua ni kipi kilichozungumzwa, lakini dalili zilionesha dhahiri hayakuwa maongezi ya kheri. Tausi alishafura kwa hasira.
Elia akamfuata huko chumbani alikokukwa ameelekea. Akamkuta mwanamke huyo akiweka sawa nguo zake na kuvua zile alizonazo ili ajiandae kwa safari.
"Unaondoka?" Elia aliuliza kwa utaratibu huku akiketi katika upande wa kitanda. Sauti ya Elia ilikuwa chini. Yenye kuthubutu kukiri kuwa imekosea.
Tausi hakumjibu. Mashavu ya mwanamke huyu yalishatota kwa machozi. Aliminya pua zake kila dakika. Na muda huo alikuwa akimaliza kuiweka sawa sidiria

iliyokuwa imeyashikilia vema matiti yake yaliyo ndani ya ujazo wa kujitosheleza.
"Tausi, unaondoka?" Elia alikariri swali....
"Unaniuliza wewe kama nani?" Sasa Tausi alijibu huku kila silabi yenye kuchomoka katika kinywa chake ikijaa mtetemeko wa wivu na hasira.
"Unachofanya unakosea!"
"Kwa kuwa wewe ulichokifanya umepatia. Elia, naomba uniache!" Kauli ya Tausi ikabeba jina 'Elia' na kulitupa lile 'Mume wangu' ambalo ndilo limezoeleka. Haikuwa ishara njema.
Mwanaume aliyeitwa na mkewe kama vile zimwitavyo ndimi za watu baki, akainuka kutoka katika ile kona ya kitanda na kusimama juu. Hatua zake zikaingia tamaa ya kumkurubia Tausi ili amguse. Sekunde hiyo, mgongo ukamkubusha kuhusu kile kikumbo kikali alichotandikwa pale katika mlango wa jiko. Akarejea tena kuketi shauri ya woga.
"Tausi, yule mwanamke simpendi. Ni basi tu!" Akauvesha magwanda mdomo wake kuingia katika vita vya kuitetea ndoa. Silaha ikiwa ni uongo.
"Elia, mimi naomba uniache. Naomba sana! Usiniongeleshe!!" Tausi alijibu. Kuna namna kule

kunyeyekewa kulianza kumpa raha. Na alitamani kuendelee zaidi.

Ukimya wa sekunde sita ukatosha kabisa kukivisha ujasiri kiwiliwili cha Elia, akaamka kwa awamu nyingine. Bila kutafakari sana, akamsogelea Tausi wake. Liwalo na liwe.

"Nisikilize mke wangu..." Pigo la kwanza la Elia likaenda katika sikio la kushoto mwa Tausi aliyekuwa amemwachia nyuma  mgongo wake mpana.

Bibiye kimyaa. Hatikisiki shingo wala kona ya kiwiko. Ngozi imemwingia ubaridi mithili ya chura aliyekosa tundu akazama kwenye mdomo wa kiatu.

Elia akachukua mkono wake na kumwekea begani. Moyo wa Tausi ukakwaa tuta katika mwendo. Ukapunguza kasi. Hasira zilianza kumshuka.

Elia aliligundua hilo baada ya kuona mke hazungumzi lolote....

Baada ya sekunde kumi na tano za ubembelezwaji uliojaa ahadi, viapo na ukanushi wa hali ya juu kutoka kwenye kinywa cha mwanaume, hasira zikapoa kwa yule aliyekuwa amekwisha kuvaa ili aondoke. Safari ikafa alipokigeuza kiwiliwili chake. Wakatazamana kwa

majira mafupi ya dakika, viwiliwili vikanatana. Midomo nayo ikaona ya nini ichelewe?

Ikasogeleana. Ndimi zikazama kwenye mazungumzo ya kina.

'Suzi ni nani?'

Ulimi wa Tausi ulihoji ukiteleza katika kuta za mashavu ya Elia.

'Suzi yupi?'

Ule wa Elia ukajibu.

'Suzi... Humjui?'

Wa Tausi ulizungumza huku ukiwa ukizungusha kulipapasa paa la kinywa cha Elia.

'Subiri baadaye, tutaongea!' Ule wa Elia ukasitisha maongezi, ukijichomoa kinywani na kutua kwenye shingo ya Tausi. Hesabu za Kifizikia juu ya kiwango sahihi cha mtetemeko wa misuli ya binadamu zikaanza kuvunjwa taratibu. Mwanamke pumzi zilimtoka mithili ya anayekimbia. Magoti yakamlegea. Uzito wake ukaamza kumuelemea Elia...

Kama waangendelea kusimama, zoezi lingesababisha mmoja wao aiangukie sakafu, ama wote kwa pamoja. Wakakiwahi kitanda. Chaga zikalalamika na

kuthibitisha kuwa, 'Naam... Swadakta! Nimezipokea kilo za kutosha!'
Hizi kilo zikaanza kupungua taratibu. Gauni refu jekundu likatupiwa karibu ya uvungu. Ikafuata ile iliyokuwa ikiwekwa sawa ile.... Yenyewe ilikuwa nyeusi. Mwanamke mnene mwenye tumbo la shibe na umbile la kibantu akawa yuko wazi. Utamwambia nini Elia mbele ya muonekani huo akakuelewa?
Mbele ya kuutafuta msamaha kwa jasho tena?
Zile chaga zilizokuwa zikilalamika kwa kuipokea miili. Zikaingia rasmi kwenye kilio...
Kilio cha kutikiswa bila ya huruma.
Maandalizi ya mlo wa usiku yakakomea hapo. Kwenye kipindi cha mapumziko mafupi kabla ya kuendelea, ikapigwa simu kwa mmiliki wa mgahawa uliopo barabarani. Akaelekezwa eneo na kuagizwa mapochopocho. Angalizo kubwa aliloachwa nalo. Ni kupiga simu akifika tu nje ya geti...
Mchezo ukaingia kwenye mzunguko wa pili...
"Naam, huyu nd'o Elia wangu sasa!" Ubongo wa Tausi ukazungumza kwa tabasamu.
Narudia, ni ubongo ndiyo uliozungumza. Mdomo ulikuwa kwenye wajibu mwingine wa kutoa kelele.

Tazama... Kuna mtu sasa anataka nianze kumueleza ni kelele gani!

Wawili hawa waliendelea na shughuli yao, bila kujua, kuwa, nje, nje ya nyumba yao, kabla ya yule waliyekuwa wakimtegemea kufika hajafika, alifika kiumbe mwingine..

Gauni fupi. Chini kandambili za uani. Shari imejaa. Kichwani wigi alizoea kulivaa hakuwa nalo. Kuashiria huko alikokuwa huko, alitoka bila ya kujipanga....

Hatua mosi, hatua pili, akalifikia geti kutoka kwenye pikipiki.

Akaitoa simu yake, akaenda mpaka kwenye namba ya mlengwa. Alipotaka kuipigia, akasita. Kisha akaghairi kabisa na kuamua kugonga hodi.

Huyu niliyemwita kiumbe mwingine na nyote mkaridhia, lipo jambo lisilo jema alilokuwa amelidhamiria!

# 11

"Si tulimwambia akifika atupigie? Sasa geti anagonga la nini?" Elia alifoka huku macho ameyatumbua. Yuko chali. Chini ya Tausi aliyekuwa kwa juu yake.

Walikuwa kwenye hekaheka za kulitimiza agizo mama la binadamu kuumbwa kwa jinsi mbili tofauti: mwanaume na mwanamke. Jukumu ambalo, sio kwa binadamu tu, viumbe wote wanalitii kwa unyenyekevu kabisa. Na katika mazingira yenye utulivu.

Ni huo utulivu nd'o uliokosekana. Ukasababisha Elia akunje uso huku akimsogeza mkewe pembeni na kujiinua kitandani. Akawa mwenye kuitafuta suruali yake huku lawama nzito zikichepuka kutoka kinywani mwake.

"Agh! Mijitu mingine bwana, sijui akili zao zipo katika matundu ya makalio? Kwamba kila wakishiba na kwenda kujisadia wanazipunguza. Nini sasa hiki?"

Hakieleweki ni kitu gani kilichokuwa kimekwaza Elia. Vyovyote vile alivyokuwa akitamani iwe...

Ama kwa simu kupigwa, au kupuliziwa tarumbeta, lazima tu angepaswa kuusimamisha ule mchezo mtamu na kwenda kumsikiliza huyo aliyekuwa mlangoni. Na akili yake ilikuwa ikimtuma ni mleta chakula ambacho alikiagiza.

"Acha tu niende mimi!" Kabla ya Elia kuipata nguo yake, Nyayo za Tausi zilikuwa sakafuni kuufuata mlango. Alishajitundika gauni lake jekundu mwilini.

Mume akasalia kinywa wazi asijue la kutenda. Alipoombwa pesa, akagoma na kusema ni usiku. Angeenda yeye tu.

"Sasa beeeeeib, mtu wa watu hapo nje asimame tu... Kweli?" Hii 'Kweli?', ilitokea mashavuni. Sauti ndani ya mdeko uliopitiliza. Macho legevu utasema mwendo wa ng'ombe mwenye nundu aliyetelekezwa jangwani kwa kufananishwa na ngamia.

Utiifu ukamvaa Elia. Akachomoa kiasi cha shilingi elfu ishirini katika droo na kumkabidhi mkewe.

"Halafu hawana adabu hata kidogo na wateja, ugongaji gani huo wa kwa nguvu bila kupumzika?" Tausi alipokuwa akiishia kwenye kona ya kuifikia sebule, aliacha nyuma sauti ya Elia iliyokuwa bado ndani ya malalamiko.

Milango ilifunguliwa, Tausi akatoka nje, vyote hivyo Elia alikuwa akivisikia, akiwa kwa ndani, kisha, badala ya kuzisikia sauti hizo zikijirudia kwa mara ya lili kuashiria kuwa huyo aliyetoka anarudi ndani.

Zikazuka sauti mpya za mabishano yaliyokuwa yakiendelea.

"Pumbavu kabisa! Sasa wamefikia kufokeana na mke wangu!" Elia alizungumza kwa jazba huku akiutoa nje mwili wake kwa kuututumua. Huku simu ameishika mkononi. Akidhamiria kumshikisha adabu huyo kijana aliyetumwa kuwaletea chakula. Kuu zaidi ya yote, akiwa amepanga kutokumlipa na kumfukuza kabisa. Chakula kingekuwa basi! Wakale wao na bosi wao asiye na umakini hata kushindwa kuajiri watu wenye nidhamu ya utendaji.

Kufikia sebuleni. Hisia zake zikaanza kugongwa makwenzi ya kuumbuliwa. Sauti mbili tofauti zilizokuwa ndani ya mzozo, hakukuwa na hata moja ya kiume. Zote zilikuwa ni sauti za wanawake.

Akasimama asikie vizuri hicho walichokuwa wakikigombania...

"...Sio mumeo huyu! Unanga'anga'nia mumeo mumeo! Wewe mwanamke gani wewe wa kulazimisha ndoa?" Hii ilikuwa ni sauti ya mkewe. Na aliifahamu.

'Mke wangu anagombania mume na nani?'

Elia akajiuliza, baada ya sekunde moja akagundua mume ni yeye.

'Suzi? Suzi amekuja mpaka kwangu?'

Hili sasa likamtia hofu. Isingekuwa rahisi kwake kujitetea. Akabadili uelekeo haraka sana kulikimbilia kochi lililokuwa karibu na dirisha.

Akayapa utulivu mpya masikio yake huku akiendelea kutafakari.

'Lakini, mbona Suzi hakuwahi kuja? Sijamleta kabisa hapa. Amepajuaje?'

Akajikosoa kwa kuweka kumbukumbu zake sawa kuwa, hakuwahi kuthubutu kumfikisha Suzi anapoishi.

"...Na umwambie kabisa. Kama alivyotia mimba, basi na ajue kuilea!!" Sauti ikapaa kutoka huko nje na kumfikia.

'Mungu wangu... Suzi ana mimba!?'

Sasa moyo wa Elia uliokuwa ukicheza kwa kuyumbayumba, ukaningia rasmi kwenye mneso wa kuruka juu na kushuka.

Akaanza kutafakari majibu atakayoyatoa kwa jamii kuieleza ni Bailojia gani ya kulala kitandani na mkeo kisha mimba aipate mwanamke mwingine?
Lakini, sauti ya huyu mwanamke aliyekuwa akilalamika kuhusu mimba, haikufanana hata kidogo na ile Suzi.
'Au amelewa?' Bado aliendelea kujichemsha katika sufuria ya mashaka na kufikiria mengi. Akawaza labda sauti hiyo ni ya Suzi mwenyewe, isipokuwa tu, atakuwa amekunywa kilevi.
Hajawaza na kuwazua, purukushani za kusukumana zikaanza kusikika huko nje.
Wanapigana!
Ndivyo alivyowaza Elia. Akatoka mkuku mkuku kwenda kuamua. Huo haukuwa muda wa kujificha tena.
Alimkuta mkewe akiwa juu ya mwanamke mwingine. Akaiweka ile simu mfukoni, kumuwahi na kumvuta. Tausi akakaa kando akipumua kama kiboko. Yule mwanamke aliyekuwa amekabwa, aliendelea kuhema kwa kasi na kuonekana kushindwa kuamka. Sura yake wala haikuwa na wenyeji wowote kwa Elia. Hakumjua ni nani.

"Elia... Mi..mi.. mimi naenda kwetu. Siwezi. Nimechoka!" Tausi akaanza kushusha lawama huku akitamani kulia.

Yule mwanamke aliyekuwa akipigwa, hali yake haikuonekana kuwa sawa. Bado alikuwa chali na pumzi zikiendelea kumkimbia na kumvamia kwa fujo. Elia alimshika mkono amuinue huku akimtazama vizuri...

Huyu ni nani?

Swali la msingi kabisa kati yetu sote! Hususani sisi tuliodiriki kumsingizia Suzi wa watu.

Mola atusamehe!

# 12

Kumbukumbu zake zilikuwa nusu. Ni mtaa ambao aliwahi kufika. Lakini ufanani wa nyumba mbili zenye kutazamana ulimchanganya.

"Hivi niliingia hii ya kushoto, au ya kulia?" Alijiuliza wakati akishuka kutoka juu ya pikipiki.

Ni mwanamke mjamzito. Mimba ya miezi minne. Ilikuwa bado changa, ila tayari ilianza kumletea kashikashi.

Mara zote alizojaribu kumpigia simu baba mwenye tumbo husika, alipewa ahadi kadha wa kadha kuwa angetumiwa gharama za hospitali. Zilidumu kuwa ahadi mpaka pale alipopotea mazima. Kila alipopigiwa, hakupatikana. Na mara nyingi simu yake kuwa ndani ya matumizi.

'Namba unayopiga, inatumika kwa sasa, tafadhali, jari....' Sauti ya huyo dada wa huduma ilimkera mpaka akaanza kuipenda. Shauri ya kuisikia mara kwa mara.

Wawili hao walikwaana baa tu. Wote wakiwa wamelewa. Wako chakali kwa pombe. Fahamu zao

zikisimamiwa na viungo vya siri. Namna pekee waliyoiona ingefaa kuwaweka sawa ni kukikimbilia kitanda. Wakazoana huko walikokuwa. Mpaka kwenye nyumba ya mwanaume.

Ulikuwa ni usiku mmoja tu. Na ilipaswa iwe hivyo. Pambano la mara moja kisha kila mmoja aendelee na hamsini zake. 'One night stand'. Waitavyo vijana wenye unasaba wa ndimi za Kiingereza chenye uhuni.

Wala hazikuwa hamsini kamili, kila mmoja akachukua arobaini. Ishirini zikasalia zikiwasubiri.

Na aliyeanza kuziona, ni huyo mwanamke. Damu za mwezi zilipoamua kubeba utoro wa kudumu. Kichefuchefu kikawa ndiyo kiranja wa darasa. Kila alichothubutu kukibandika katika kinywa, kilipolikaribia koo tu, kikatoka.

Tayari alikuwa nje ya mlango wa huyo mwanaume tapeli. Baradhuli asiye na huruma kwa damu yake halali. Aligonga geti kwa nguvu na hasira kuitangaza nia yake. Alichoka. Alichoka kupotezewa na mtu ambaye walishiriki kwa pamoja kulimwagia mbegu shamba, halafu akakimbia wakati wa kulipalilia.

Mara, pasipo kutarajia, anatoka mwanamke mweusi, mnene, macho ameyatumbua.

Naye akayakaza ya kwake!
"Unataka nini?" Swali la kwanza kutoka kwa mwanamke aliyekuwa ndani ya gauni jekundu likamfikia.
"Huyo mwanaume huko ndani, yupo?" Akamuulizia mtu aliyekuwa akimhitaji.
"Usiseme mwanaume! Sema mume wangu!" Karipio lenye agizo likamkaba.
Naye akaja juu, "Mumeo kivipi? Mbona aliniambia hajaoa?"
Labda ni kiburi cha mimba changa. Alishindwa nini kuulizia? Pengine kungemsaidia na kugundua kuwa amekosea nyumba...
Msichana huyu akaingia kwenye mzozo mkali wa maneno na Tausi. Mke wa Elia. Tausi akifikiria aliye mbele yake ndiye Suzi.
Maneno yalipowakauka. Vikahamia vitendo. Yule mwenye nguvu ndogo akawekwa chini. Akakabwa. Akakwidwa. Akakaliwa tumboni mwake na zile kilo nyingi za kisukuma.
Wa kuzihimili vile ni Elia peke yake, tena juu ya kitanda chenye godoro laini. Sio pale chini! Kwenye ardhi ngumu!

Nguvu zikaanza kumkimbia, pumzi kumponyoka, uwezo wa kuona ukabadilika. Vitu havikuwa na rangi tena, ni nyeusi kwa nyeupe. Aliyekuwa juu yake aliendelea kuing'ang'ania shingo! Kila alipojitahidi kutamka neno, hakuna ambalo lilichomoka hata kwa silabi moja.

Mpaka alipofika mkombozi ambaye hakuweza kumfahamu vizuri kwa sura, tayari roho ilikuwa katika njia panda ya uhai, kuumeni dunia, kushoto akhera.

"Umeua!" Ndiyo ilikuwa kauli ya Elia baada ya kujaribu kumshika mkono mwanamke huyu na kugundua umelegea. Mkono haukuwa mgumu tena.

Tausi akashika kichwa chake juu kwa majuto. Akamsogelea yule binti na kumwita kwa jina alilokuwa akilikumbuka, Suzi.

"Suzi... Suzi... We Suzi!"

Elia anamshangaa. Nd'o anamfungua. Huyu si Suzi bibiye! Mimi mwenyewe simfahamu!!!

Macho yanamtoka mwanamke. Mara mbili ya ule ukubwa wake. Kijasho kikaamvaa cha kutosha, zaidi ya kile kilichokuwa kimesababishwa na hekaheka za mapigano.

Wanandoa hawa wakazama kwenye mzozo. Hawaelewi wanafanya nini. Wakaanza kuangushiana lawama.
Elia akatangulia kumponda mkewe kwa pupa yake ya kuamua kutenda kila jambo bila busara ya uvumilivu. Tausi pia akalalamika mumewe amezidi kuwa msaliti. Akidai pengine na mwanamke huyo ni wake.
Elia anakana. Naye anapapasa kwa kujitetea, anagusia kuhusu zile picha alizowahi kutumiwa. Anahoji...
Mbona mimi sijachukua maamuzi ya kukurupuka?
Mara, linakuja sikio la tatu, hili, ndilo lililokuwa limeleta chakula. Kabla ya sikio hili kuwafikia. Wakapanga walilishe uongo. Kuwa yule aloyedondoka ni ndugu yao. Hivyo wangemuomba huyo kijana awasaidie wambebe wamuingize ndani. Na huko ndiko wapange cha kufanya.
Tayari yalishamwagika. Si kuzoa tena, ni kupangusa ama kufuta kabisa.
Sikio hili likawasikia. Likawatii. Likawasaidia. Lik'enda zake.
Chakula tena hakikulika. Chini hakukukalika.
Wafanye nini?

Kesi iliyokuwa mbele yao ni kubwa. Walilia kwa pamoja, wakakumbatiana. Majira yote ya mwaka yakawapitia. Kiangazi kwa masika. Ukame kwa vuli.

Majira hayakwisha... Likasogea lingine geni... Hili halikueleweka. Lilikuja na viumbe wenye pingu mkononi. Kauli mdomoni...

"Sisi ni askari polisi kituo cha kati, kuanzia sasa mko chini ya ulinzi kwa kosa la mauaji!"

# 13

Alishakata tamaa. Kile alichotoka kukizungumza katika simu saa moja iliyokuwa imepita alikihesabu kama kifunga maongezi kati yake na Elia. Aliwaza kumfuta mwanaume huyo katika ukurasa wa maisha yake. Kama kipo ambacho aliwahi kukitamani na hajakipata kutoka kwa mwanaume huyo, basi aliamua kukisahau na kutokifikiria tena.

Kwa mara kwanza tangu mwanzo wa kuzama ukubwani, Suzi anajikuta akikata shauri la kuachana na mwanaume.

Suzi amekuaje?

Hata rafiki yake aliyekuwa pamoja naye hakuweza kumwelewa. Shogaye alibadilika ghafla. Leo hii Suzi wa kukaa na kuacha kula akimtafakari mwanaume? Suzi huyu uyu wa kupigiwa simu na mwanaume mwingine, akiwa juu ya kifua cha mwanaume mwingine, akaulizwa na huyo mwingine aliyepiga kwanini analia na kujibu yupo msibani...

Suzi huyuhuyu?

Tangu aliporudi na kujilaza pale kitandani, hakuamka. Simu yake iliita kutoka kwa watu tofauti, hakuna ambayo aliitikia. Juma bodaboda, Hamisi muuza vitambaa Tandika, John fundi simu.... Wote hawa hawakuwa na thamani yoyote kumlinganisha na yule mwanaume ambaye alimhifadhi kwa jina la hadhi...

Mr. Elia Maige! Mmiliki wa kampuni ya usambazaji samaki. Mwanaume mtanashati, mwenye hela.

Ndani ya dakika chache, simu kutoka kwa mtu huyo aliyekuwa ndani ya fikra zake ikaingia. Akawahi kuipokea. Akiwa kwenye bashasha la mategemeo mema, anasikia watu wakihangaika kubishana kuhusu maiti. Anayasikia majibizano kati ya Elia na mkewe. Anasikia namna anavyoitwa kwa majina machafumachafu. Namna anavyomwagiwa sifa mbovu na Elia huku akikanwa. Anaumia. Anagundua ni simu tu ingekuwa imejipiga ikiwa mfukoni. Yale mazungumzo hayakuwa mazuri. Yalijaa uhalifu. Anayarekodi. Kisha anakata simu. Anayahifadhi.

Akili ya Suzi ilishavurugika. Aliamini ugali wake umemwagwa, sasa ni wajibu wake, mboga kuimimina mavumbini.

Akaichukua rekodi ile ya sauti na kuituma kwenye makundi ya Whatsapp. Akisindikiza na majina ya wahusika. Bwana na Bibi Elia Maige!

Haukuwa wivu tena huu, bali chuki.

Ni kweli, polisi waliwahi na kuwakamata watuhumiwa usiku uleule. Elia na mkewe waliwekwa mikononi mwa dola. Suzi akiamini kikombe amekiepuka.

Mkono mrefu wa sheria ukamfikia asubuhi iliyofuatia. Naye akatupwa ndani! Huko, aliingizwa kwa lengo la kutakiwa kutoa ushirikiano.

Kuulizwa, aliipata vipi ile rekodi ya sauti?

Ila, jina lake lilipojazwa katika rekodi, zikakutwa RB nyingi zilizokatwa dhidi yake. RB zenye sababu lukuki... Huyu kaibiwa mume halali wa ndoa, huyu katishiwa kupigwa chupa ya uso baa... Mbele ya yote, jina la mlalamikiwa likasimama moja pekee, Suzi Chitete!

Mahabusu hayachagui wa kummeza, Suzi akaswekwa ndani kwa ajili ya upelelezi zaidi. Alionekana kujaa harufu ya uhalifu.

Na baada ya uchunguzi wa muda mfupi, takribani miezi mitatu, huo ni muda mfupi sana kwa aina ya kesi yao, uchunguzi uliowafanya baadhi ya ndugu kufunga safari kadhaa ndefu za kwenda rudi, kutoka Mwanza

mpaka Dar Es Salaam, wanandoa wawili wakaachiwa huru kwa kukutwa hawana hatia. Suzi akasalia ndani. Atetewe na nani?

Elia na mkewe walipokutana kwa mara nyingine baada ya kung'atwa na mbu wa kutosha, na kulionja joto la vyumba vyenye madirisha madogo mithili ya macho ya mtu anayekonyeza, wakaingia upya katika viapo vya kuepuka kusalitiana. Namba ya Suzi ikafutwa katika simu. Tusi lile lililowadhalilisha wakalitupilia mbali kabisa!

Wakati wao wakifanya hilo, alikuwepo askari, askari polisi, mwanaume, kituoni, akihangaika na mafaili huku na huko, kila iitwayo siku, kushughulikia kesi ya Suzi, ili atoke, akiwa ameahidiwa kupatiwa kila akitakacho na binti huyo...

Na huo, ukawa mwanzo wa mkasa mzito wa kipelelezi uliohusisha mikono ya binti machepele, Suzi Chitete.

Ni mkasa upi?

Hata wadudu ardhini wanaisubiri kalamu ya Abyas Mzigua!

# MWISHO!